

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

Simu: 2552225/2552082

Fax: 2552586/2552504

Unapojibu tafadhali taja:



Ofisi Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
S.L.P. 148,
TUKUYU.

Kumb.Na.RDC/F.4/09/49

24/12/2018

- Wakuu wa Idara wote
- Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo
- Maafisa Tarafa wote wilaya ya Rungwe
- Viongozi wa Wafanyabiashara (W)
- Viongozi wa Taasisi za Dini.
- Wakuu wa Taasisi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali.
- Polisi na Magereza
- Wafanyabiashara wote

YAH: KUKUMBUSHA SIKU MAALUMU YA USAFI WA MAZINGIRA (KITAIFA) KILA JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI.

Husikeni na kichwa cha habari cha hapo juu. Ninawakumbusha kwa mara nyingine tena kuwa kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi ni Siku Maalumu ya Usafi wa Mazingira Kitaifa. Kwa mwezi huu wa Disemba 2018 Jumamosi ya mwisho wa mwezi itakuwa 29/12/2018.

Sote kwa pamoja tunatakiwa kushiriki kikamilifu katika shughuli hii muhimu ya kufanya usafi katika maeneo mbalimbali kwa faida yetu wenyewe. Maeneo hayo ni kama vile Ofisi zetu, Maeneo ya Biashara, Makazi, Stendi za Mabasi na Taxi, Viwanja vya Michezo na Maeneo ya wazi, Barabara na Mitaro ya maji. Shughuli itaanza saa 1:00 - 4:00 Asubuhi.

Kamati ya Ulinzi na Usalama, Viongozi wa Halmashauri, Uongozi wa Wafanyabiashara, viongozi wa Kata vijiji na Vitongoji watafanya ukaguzi na ufuatiliaji ili kuona na kuhakikisha wananchi wote wanashiriki. Hatua stahiki zitachukuliwa kwa makundi ambayo hayatoshiriki kama ilivyoanishwa kwenye sheria. Ikiwemo kutozwa faini isiyopungua Tsh 50,000/= (Elfu hamsini kwa wale watakaokaidi)

“Rungwe bila uchafu inawezekana, sote tushirikiane”

Nawatakia kazi njema.

Loema I. Peter

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

RUNGWE

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE

NAKALA: Katibu Tawala Wilaya
RUNGWE.